JARIDA MTANDAO LA

# UBUNGO YETU

TOLEO LA JULAI-SEPTEMBA 2022





MHE. KHERI JAMES
MKUU WA WILAYA YA UBUNGO



MHE. JAFFARY NYAIGESHA
MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA YA UBUNGO



NDUGU. BEATRICE DOMINIC
MKURUGENZI WA MANISPAA YA UBUNGO

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

# RC MAKALLA: OPERESHENI INAENDELEA, DAR ES SALAAM NI

- Asema Operesheni ya kukamata Panya Road imekuwa na mafanikio makubwa.

-Vituo vya polisi vikubwa kwa vidogo kufanya kazi saa 24 kudhibiti uhalifu.

- Aelekeza Kila Mtaa kuweka utaratibu wa kufanya kikao Cha Ulinzi kila wiki ya kwanza ya Mwezi.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amos Makalla amesema kwa siku nne tangu kuanza kwa Operesheni ya kukabiliana na Panya Road Mkoa upo salama Baada ya kufanikiwa kuwakamata Watuhumiwa 135 na Vifaa mbalimbali vilivyoibiwa.

RC Makalla amesema hayo wakati wa kikao kazi Cha Kamati ya Ulinzi na usalama kilichoketi kufanya tathimini ya Hali ya usalama Mkoa pamoja na kupokea taarifa ya mwenendo wa Operesheni ya kukamata Wahalifu.

Ili kuhakikisha matukio hayo hayajirudii, RC Makalla amebainisha mipango ya kudhibiti uhalifu ikiwemo Vituo vyote vya polisi kufanya kazi kwa saa 24, Ongezeko la Doria kila Kata, Kila Mtaa kufanya mkutano maalumu kujadili ajenda ya Ulinzi na usalama kila wiki ya kwanza ya Mwezi.

Aidha RC Makalla amesema mipango mingine ni msako kwa Wafanyabiashara wanaouza na kununua Vifaa vya Wizi, Kuimarisha Vikundi vya ulinzi Shirikishi, ufuatiliaji wa mienendo wafungwa waliomaliza kutumikia vifungo na msako kwenye vijiwe, majumba mabovu yasiyokamilika (Mapagala) na vibanda umiza ambavyo vimekuwa sehemu ya kukutana na kuweka mipango.

Pamoja na hayo RC Makalla ametoa wito kwa Wazazi kuhakikisha wanazingatia suala la malezi kwa kufuatilia mienendo ya watoto wao.

Operesheni ya kukamata Panya Road ilizinduliwa Septemba 15 na ndani ya siku nne imekuwa na mafanikio makubwa yaliyopelekea kukamatwa kwa Watuhumiwa 135, Wanunuzi 5 wa Vifaa vya Wizi na kupatikana kwa Mali zilizoibiwa ikiwemo Tv, Radio, simu za mkononi na vitu vingine.








# PANYA ROAD WADHIBITIWA UBUNGO.



Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Kheri James amewahakikishia wananchi wa Wilaya hiyo kuwa kufuatia matukio ya Panya Road yanayohatarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Wilaya hiyo imejipanga kudhibiti hali hiyo, hivyo wananchi waendelee na shughuli zao za kimaendeleo huku wakishirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kutoa taarifa za waarifu.

Mhe. James alitoa kauli hiyo Septemba 15, 2022 katika kikao kazi kilichojumuisha Wenyeviti wa Mitaa, Watendaji wa Kata na Mitaa wa Wilaya hiyo lengo ikiwa ni kujadili na kuweka mikakati ya kuhakikisha suala la ulinzi na usalama linaendelea kuwa ni jukumu la kila kiongozi kwenye eneo lake ikiwemo kukomesha masuala ya unyanyasaji wa kijinsia hasa kwa watoto.

Kheri aliendelea kueleza kuwa kumeibuka vitendo vya uhalifu vinavyofanywa na vikundi vya vijana wadogo maarufu kama 'Panya Road' katika mitaa mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam ambapo amesema kwa upande wa Wilaya ya Ubungo hali ni shwari na hakujaripotiwa taarifa yoyote ya vitendo vya uhalifu na uvunjifu wa amani.

Aidha, Kheri ametoa wito kwa wazazi na walezi kuhakikisha wanasimamia maadili ya watoto wao kwa kufanya ufuatiliaji wa mienendo yao kwani wanaojihusisha na vitendo vya kihalifu ni vijana wenye umri mdogo na ameagiza jeshi la polisi kukamata wahalifu hao na kuwafikisha mahakamani kwa hatua za kisheria.

"Tukiendelea kudekeza wahalifu katika mitaa yetu Nchi itaingia matatizoni, Muhalifu akikamatwa apelekwe mahakamani haraka ili akahukumiwe kwa mujibu wa Sheria"
Alisema James.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Mpigi Magoe ndugu Said Seleman Diuchile ameeleza kuwa wao kama viongozi wapo tayari kutoa ushirikiano kwa jeshi la polisi juu ya utoaji taarifa za wahalifu sugu kwenye mitaa yao ili kusaidia Wananchi kuwa salama katika shughuli zao za kila siku.

Kwa upande wake Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya Kipolisi Kimara SP Leah Ncheyeti ametoa taarifa ya kukithiri kwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya hiyo ambapo wanawake na watoto wamekua wakikumbana na vitendo hivyo kwa kiasi kikubwa.

SP Leah ameendelea kueleza kuwa vitendo hivyo vimekithiri kutokana na watu wengi kunyamazia vitendo hivyo vinapotokea katika ngazi ya familia hali inayopelekea kupoteza ushahidi muhimu wa kuwafikisha watuhumiwa kwenye vyombo vya Sheria.

Operesheni ya kukamata panya road ilizinduliwa September 15 na ndani ya siku nne imekuwa na mafanikio makubwa yaliyopelekea kukamatwa kwa watuhumiwa 135, wanunuzi 5 wa vifaa vya wizi na kupatikana kwa mali zilizoibiwa zikiwemo TV, Radio, Simu za Mkononi na vitu vingine.



## BEI ZA KODI YA PANGO KITUO CHA MABASI CHA MAGUFULI ZASHUSHWA



Manispaa ya Ubungo imeshusha viwango vya kodi ya pango katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli (Magufuli Bus Terminal) kutoka shilingi 40,000 kwa mita za mraba hadi shilingi 25,000 kiwango cha juu huku kiwango cha chini kikiwa shilingi 20,000 kulingana na eneo alilopanga mfanyabiashara.

Mabadiliko ya viwango hivyo yamefanyika baada ya Manispaa hiyo kupokea na kufanyika kazi maombi kutoka kwa wafanyabiashara waliopanga maeneo ya biashara (fremu na vizimba) katika Kituo hicho kikubwa cha Mabasi Nchini kuomba kushushiwa viwango hivyo ili waweze kumudu kulipa kodi ya pango bila kuathiri ustawi wa biashara zao.

Akiongea katika kikao hicho Mkurugenzi wa Manispaa hiyo Beatrice Dominic alieleza kuwa ombi la wapangaji hao la kushushiwa gharama za kodi limefanyiwa kazi ambapo viwango vya kodi hizo vimepunguzwa kiasi ambacho kila mfanyabiashara ataweza kumudu kulipa kodi hiyo bila shida kwani awali wapangaji wengi walikuwa wanashindwa kulipa na hivyo kuisababishia halmashauri kushindwa kukusanya mapato kama ilivyopanga.

Beatrice alifafanua kuwa kabla ya punguzo la viwango vya kodi Manispaa iliwajibika kugharamia huduma za maji, usafi ulinzi na umeme ila baada ya punguzo la viwango hivyo vya kodi kila Mfanyabiashara atawajibika kulipia huduma ya umeme kulingana na matumizi yake kama utaratibu utakavyoelekeza huku Manispaa ikiendelea kutoa huduma za Maji , Usafi na Ulinzi.

“Kila mfanyabiashara anamatumizi yake mfano mwenye majokofu na majiko matumizi yake ni makubwa kuliko anayetumia umeme kwa ajili ya kuwasha taa na kiyoyozi pekee hivyo ni vema kila mmoja akalipia kulingana na mtumizi yake” alisisitiza Beatrice

Akifafanua kwa kina mchanganuao wa viwango hivyo vipya vya kodi , Mkuu wa Kitengo cha Fedha wa Manispaa hiyo George Mzeru alisema kuwa Wafanyabiashara waliopanga Jengo la Utawala kwa Sakafu ya chini (ground floor) Tsh 25,000, Sakafu ya kwanza (first floor) Shilingi 24,500, sakafu ya pili (second floor) shilingi 24,000 na sakafu ya tatu (third floor) italipiwa shilingi 22,000

Kwa upande wa Jengo la abiria ambalo chini Lina “Basement” Sakafu ya kwanza (Mezzanine floor) itakuwa shilingi 22,500, Sakafu ya pili (second floor) 22,000 na Sakafu ya tatu (third floor) italipiwa shilingi 20,000.

Kwa upande wake Mkuu wa Kitengo cha Sheria wa Manispaa hiyo Kissah Mbilla amewataka kila Mfanyabiashara kuhakikisha analipa kodi za pango za kuanzia mwezi Julai hadi Septemba 2022 na kupewa mkataba wake, kwa atakaye kaidi atachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kusitisha mkataba wa upangaji.

Inaendelea........

Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli kilizinduliwa na kuanza kufanya kazi tarehe 24 Februari, 2021 kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma za usafiri na usafirishaji lakini pia kama chanzo cha mapato kwa Serikali ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya shilingi bilioni 4.1 zilikusanywa na kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023 jumla ya shilingi bilioni 5.04. Aidha, baada ya miundombinu yote ya kituo kukamilika kinatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 10.2 kwa mwaka



## MADIWANI WASISITIZA UKAMILISHWAJI WA MIRADI KWA WAKATI



Baraza la Madiwani Manispaa ya Ubungo limetaka kasi kubwa ielekezwe kwenye ukamilishaji wa miradi ya maendeleo na ukusanyaji wa mapato ili Halmashauri iendelee kupata hati Safi na kushika nafasi ya kwanza katika ukusanyaji wa mapato.

Hayo yamesemwa leo tarehe 12/8/2022 kwenye mkutano wa kujadili utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kipindi cha robo ya nne na kusisitiza kuwa mapato yakikusanywa kwa wingi miradi ya maendeleo itatekelezwa kwa kiasi kikubwa na kwa wakati na hivyo kuboresha huduma kwa wananchi.

Wajumbe wa baraza hilo waliendelea kusisitiza kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya kuongeza mapato na kwa vile vilivyopo Viendelee kusimamiwa vizuri.

Aidha, Wajumbe, walisisitiza Halmashauri kupitia wataalam wake na kamati ya Kudhibiti UKIMWI waweze kusimamia vyema bajeti yakusaidia na kuwahudumia watu walioathirika na maambukizi ya UKIMWI

Nae, Mstahiki Meya Mhe. Jaffari Juma Nyaigesha alisisitiza wananchi kushiriki katika zoezi la Sensa ya watu na makazi linaloenda kufanyika tarehe 23 agosti, 2022

Pia amewataka wajumbe kushiriki katika tamasha la Sensa ya Watu na Makazi kwa Wilaya ya Ubungo litakalofanyika Agosti 20,2022 katika viwanja vya Barafu - Mburahati

# MHE. KATAMBI APONGEZA VIKUNDI VYA VIJANA UBUNGO



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira,-na Wenye ulemavu, Mhe. Patrobas Katambi ameadhimisha sikukuu ya Nanenane kwa kutembelea vikundi vya vijana vilivyopo Manispaa ya Ubungo ambavyo vimenufaika na mkopo wa 10% inayotokana na mapato ya ndani ya Manispaa hiyo ambapo amevipongeza vikundi hivyo kwa kutendea haki mikopo hiyo kwa kufanya uzalishaji wenye tija na kurejesha kwa wakati.

Katika ziara Mhe. Katambi ametembelea kikundi cha Umoja ni Nguvu kinachojihusisha na utengenezaji wa mapambo ya ndani kwa kutumia unga wa gypsum na kikundi cha BRIACO kinachojishughulisha na uzalishaji wa Kripsi za viazi mbatata na kueleza kuwa dhima ya Serikali ni kuona vijana wanajiajiri kwenye shughuli za uzalishaji wakisaidiwa na Halmashauri  kwa kuongezewa mikopo isiyo na riba kama sheria inavyoelekeza.

Mhe. Katambi ametaka vijana kuwa na malengo, kusudio na shabaha katika mipango kazi yao ili waweze kuzalisha bidhaa zenye  ushindani kwenye soko la ndani na nje, kujikwamua kiuchumi, kuzalisha ajira na kuanzisha viwanda kwa kutumia elimu na ujuzi waliyonao kwani vijana ndio nguvu kazi ya jamii na Taifa kwa ujumla.

Kutokana na utendaji kazi mzuri wa vikundi hivyo, Mhe. Katambi ameielekeza Manispaa ya Ubungo kuviongezea kiwango cha mkopo vikundi

Aidha Mhe. Katambi ameeleza kuwa "Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya mwaka 2012, vijana wanakadiriwa kuwa nusu ya idadi ya watu wote kwa maana hiyo ni kundi muhimu lenye maarifa, ujuzi na usomi,nguvu kazi kwa ujumla hivyo sisi kama serikali lazima tuwekeze  nguvu katika kulisaidia kubadilisha mitazamo waliyonayo, kuwahudumia kulingana na mahitaji yao ili waweze kujitegemea na kufanya majukumu ya kimaendeleo"

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo Beatrice Dominic amevipongeza vikundi hivyo kwa kazi nzuri na kuahidi kuwaongezea nguvu ikiwemo kupata eneo la kudumu la kufanyia kazi, kutangaza bidhaa zao  pamoja na kutumia bidhaa zao kwenye miradi ya Halmshauri.



# RAIS KAUPIGA MWINGI, WATUMISHI UBUNGO WAMSHUKURU





Watumishi Manispaa ya Ubungo wamemshukuru Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kwa utendaji kazi wake ikiwemo kuboresha maslahi ya watumishi wa umma kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu aingie madarakani.

Akiongea kwa niaba ya Watumishi wa Manispaa hiyo Naomi Masangopole mbele ya waandishi wa habari leo agosti 5, 2022 na kueleza mafanikio ambayo Rais ameyafanya kwa kipindi Cha mwaka mmoja ikiwa ni pamoja na ongezeko la mishahara kwa watumishi wa umma, punguzo la madeni kwa upande wa mikopo ya Elimu ya juu ambayo watumishi wengi walikua wanadaiwa,

Watumishi wameendelea kumshukuru Rais kwa kupandisha madaraja watumishi ambapo kwa Manispaa ya Ubungo jumla ya watumishi 2199 wamepandishwa madaraja ndani ya mwaka mmoja na kuleta watumishi wa ajira mpya 68 kwa kada mbalimbali.

Pia, wamempongeza Rais kwa ongezeko la mishahara la asilimia 23.3 ambalo limelenga kuwainua wenye viwango vya chini vya mishahara na kueleza kuwa jambo hilo ni kubwa kwani linaendelea kutengeneza usawa baina yetu na kuongeza ari ya kufanya kazi

"Sisi kama watumishi tunamuahidi mheshimiwa Rais kuendelea kuchapa kazi kwani tunamuelewa dhamira yake" waliahidi watumishi hao.

Aidha, watumishi hao wamewapongeza viongozi wa Wilaya hiyo wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi kwa uongozi wao makini katika kumsaidia mheshimwa Rais kutekeleza majukumu yake ya kuhudumia wananchi hususani usimamizi wa miradi na ukusanyaji wa mapato.

Pia watumishi hao wametumia nafasi hiyo kuwakumbusha watumishi wa umma, viongozi wa dini na wananchi kwa ujumla kushiriki katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi litakalofanyika tarehe 23.8.2022 kutokana na umuhimu wake kwa maendeleo ya Taifa letu.

# KATIBU MKUU UVCCM TAIFA ARIDHISHWA NA UWEZESHWAJI WA VIJANA KUPITIA MIKOPO YA 10% YA HALMASHAURI

Katibu Mkuu Umoja wa vijana Taifa (UVCCM) Ndg. Kenani Kihongosi ameipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa uwezeshaji mzuri kwa vikundi vya vijana kupitia mikopo ya 10% ya mapato ya ndani ambapo kupitia mikopo hiyo vijana wengi wanajipatia kipato na kuzalisha ajira kwa vijana wenzao.

Pongezi hizo alizitoa septemba 10, 2022 wakati alipotembelea kikundi cha vijana cha UMOJA NI NGUVU kilichopo katika Halmashauri hiyo kata ya kibamba kinachojishughulisha na utengenezaji wa mapambo ya ndani kupitia unga wa gypsum na kueleza kuwa kutoa mikopo hiyo ni kutekeleza kwa vitendo dhamira ya Mheshimiwa Rais  wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha vijana wanawezeshwa.

Kenani  amesema kuwa, Kwa mujibu wa taarifa ya kikundi hicho, Vijana hao baada ya kupata Mkopo wa Halmashauri wa shilingi Milioni 37.5  wameboresha uzalishaji wa bidhaa za kiwanda chao, kuongeza wateja , kufanya marejesho kwa wakati na  kulipa kodi za Halmashauri na TRA.

Kenani amekiri kuwa, Moja ya changamoto kubwa kwa vijana wanaopata mikopo hii hawafanyi marejesho



lakini kikundi hicho kinafanya marejesho vizuri na wana mpango wa kumaliza mkopo wao kabla ya muda uliopangwa, "nawapongeza sana".

"Vijana wakiwezeshwa wakafanya kazi za uzalishaji mali na biashara ni walipaji wazuri wa kodi za serikali na nchi itapiga hatua kubwa kimaendeleo" alieleza Kenani.

Aidha, amesema pamoja na mafanikio ya kikundi hicho ameitaka Halmashauri kuhakikisha vijana hao wanasaidiwa kutatua changamoto zao hasa ya kupata gari kwa ajili ya kusafirishia bidhaa zao kwa wateja "na hili najua lipo ndani ya uwezo wenu kupitia mapato yenu ya ndani, nimetembelea vikundi vingi sana lakini kikundi hiki kinaweza kuwa cha mfano katika kuitendea haki mikopo hii kupitia mapato ya ndani"

Wito wangu kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii ni kuendelea kutoa elimu kwa vijana namna ya kupata mikopo hii kwa kuwaelekeza vitu vya kuzingatia kwa ajili kupata mikopo hiyo ili tuwe na vijana wengi wanaojishughulisha na kutoa ajira kwa vijana wengine.

# UHARIBIFU WA MAZINGIRA UBUNGO SASA BASI

Kama yalivyo maeneo mengine Manispaa ya ubungo imekuwa na uharibifu wa mazingira unatokana na uchiimbji holela wa mchanga kwenye mito na maeneo mengine na hivyo kupelekea manispaa hiyo kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto hiyo kwa kuhakikisha watalaamu wa mazingira, wenyeviti na watendaji wa kata na mitaa wanalinda mazingira.

Hayo yameelezwa kwenye kikao  kazi cha kuwasilisha ripoti ya tathmini ya uchimbaji holela wa mchanga kilichojumuisha wataalamu toka Bonde la Wami/Ruvu, NEMC, Afisa Mazingira, Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti na Watendaji wa Kata na Mitaa Manispaa ya Ubungo lengo ikiwa ni kudhibiti uharibifu wa mazingira ambao unaendelea kwa sasa kwenye maeneo tofauti ya manispaa hiyo.

Akiongea kwenye kikao kazi hicho Dkt. Elizabeth Mshote Mwenyekiti kikosi kazi Mkoa wa Dar es Salaam alieleza kuwa sheria ya usimamizi wa rasilimali za maji Na. 11 ya mwaka 2009 inazitaka Bodi za maji za mabonde nchini Tanzania Bara kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazofanyika ndani ya hifadhi za vyanzo vya maji kama vile mito, mabonde, maeneo oevu, maziwa, chemchemi na mabwawa.



Mshote aliendelea  kueleza kuwa kutokana na uchimbaji holela wa mchanga katika mito na mabonde na kwakuwa kumekuwa na uhitaji mkubwa wa mchanga ambao unatumika kwa ajili ya kujengea miundombinu mbalimbali yakiwemo majengo ya Umma na binafsi na miradi mingine kumekuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira hasa kwenye mito na mabonde.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Kheri James amewataka watendaji wa Kata na Mitaa pamoja na Wenyeviti wa Mitaa kuhakikisha wanadhibiti na kuyalinda mazingira juu ya uchimbaji holela wa mchanga.

Aidha, James amesema kuanzia ngazi ya Halmashauri, NEMC, Bonde Wami, Viongozi wa Kata na Mitaa kila mmoja anawajibu wa kufanya juu ya udhibiti wa mazingira.

James amewataka watu kuacha tabia ya kuchimba mchanga kiholela kwani kufanya hivyo kunapelekea uharibifu wa mazingira tena unaopelekea kupoteza makazi ya watu. Na amesema mtu yeyote atakayefanya hivyo atachukuliwa hatua za kisheria na kama ni kampuni basi itafungiwa.

Mbali na hayo Mhe. James amelitaka jeshi la polisi kuhakikisha watu hao wanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria kwani kosa la uharibifu wa mazingira ni sawa na makosa mengine ya uvunjifu wa sheria.

“Tusipoipambania vizuri vita ya udhibiti wa mazingira vita zingine zitatushinda. Hakuna uchumi bila mazingira, hakuna utalii bila mazingira, hakuna diplomasia bila mazingira, hakuna siasa bila mazingira lindeni mazingira” Alisema James.

## SHIRIKA LA OCODE LAJENGA DARASA LA WANANAFUNZI WA AWALI




Shirika la OCODE TANZANIA limekabidhi chumba kimoja cha darasa la mfano kwaajili ya wanafunzi wa awali, viti 16, meza Tatu na zana za kufundishia vyenye thamani ya shilingi milioni 39 katika Shule ya msingi Kiluvya iliyopo Kata ya Kibamba Manispaa ya Ubungo lengo ikiwa ni kuhamasisha wanafunzi kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Akiongea katika hafla hiyo ya kukabidhi miundombinu hiyo Mkurugenzi wa OCODE Bw. Joseph Jackson amesema sambamba na ujenzi huo wamefanikiwa kutoa mafunzo ya mbinu na zana mbadala za kufundishia iitwayo jifunze kwa walimu wa darasa la awali, la kwanza, la pili na la tatu ili kuwezesha wanafunzi kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Bw. Jackson ameeleza kuwa mbinu hiyo imesaidia wanafunzi wengi kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa muda mfupi kwa shule za msingi Kibwegele, Malambamawili, Goba na Kiluvya na ametoa wito kwa Manispaa kuendeleza mbinu hiyo kwa shule zingine zilizobaki.

Aidha, ameeleza kuwa zoezi hilo la ugawaji wa vifaa hivyo limeambatana na kauli mbiu isemayo "Ulinzi na Usalama wa watoto ni jukumu letu sote tupaze sauti kupinga ukatili dhidi ya watoto wetu sote" kwani watoto wamekuwa wahanga wa vitendo vya ukatili na

hivyo kudhoofisha ustawi wao na haki zao za msingi.

Bw. Jackson ameendelea kueleza kuwa kwa muda wa Miaka minne mfululizo imekuwa ikishirikiana na Manispaa hiyo kwa kujenga shule za awali katika Shule ya msingi Kibwegere, Malamba Mawili, Goba na Kiluvya kwa gharama za Shilingi milioni 113.3.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Kheri James amelipongeza Shirika hilo na kutoa wito kwa wadau wengine kuendelea kuisaidia jamii kama ambavyo wamefanya OCODE kwani jukumu la kujenga jamii ni letu sote sio Serikali pekee.

Kheri ameitaka jamii kutofumbia macho ukatili wa watoto kwani ukatili huo usipodhibitiwa juu ya watoto wetu wataendelea kunyanyasika, pamoja na changamoto za maisha zilizopo ni lazima wazazi na walezi tutenge muda wa kuzungumza na watoto ili kujua nini wanapitia , matarajio yao na ndoto zao ili kufanikisha maisha yao ya baadae.

“Mapambano dhidi ya ukatili wa watoto ni wajibu wa kila mmoja wetu kwani mtoto anayefanyiwa ukatili atatendea wengine ikiwemo kujihusisha na uhalifu katika jamii” Alisema James

Nae Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo Bi. Leah Linus Sanga amelishukuru shirika la OCODE kwa msaada wao mkubwa na kueleza kuwa Shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 2,109 na jumla ya vyumba vya madarasa 11 ya msingi na darasa 1 la awali kutokana na wanafunzi waliopo kuna uhitaji wa vyumba 13 vya madarasa.








Anwani
Za makazi
IMEANZA RASMI
UBUNGO
NJETENI ROAD
KINZUDI ROAD
TUTOE USHIRIKIANO
KWA KUTOA TAARIFA YA
Jina la mmiliki nyumba/kiwanja
Jina la mpangaji
Kitambulisho cha NIDA
Namba ya Simu
Namba ya Kiwanja
Hakikisha unafikiwa na umepata namba ya nyumba hata kama hujajenga.
Wataalamu watakaopita wana vitambulisho na watapita na Mjumbe
Ubungo yetu fahari yetu


Halmashauri ya
Manispaa ya Ubungo
Sensa ni Msingi wa Mipango ya Maendeleo,Shiriki kuhesabiwa, tuyafikie Maendeleo ya Taifa
TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa
TAARIFA
ZITAKAZO
HAKIKIWA
|Namba ya Nyumba
|Taarifa za mmiliki wa Anwani
|Taarifa za wategemezi wa Anwani
|Aina ya jengo
|Matumizi ya jengo/kiwanja
|Taarifa za anwani tegemezi
|Jina la barabara
|Jina la kata, Mtaa, Shehia, Kijiji na kitongoji
|Taarifa za huduma muhimu.
ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI
10
28
Taarifa hizi zimebandikwa kwenye ofisi zote za Mitaa, Ewe Mwananchi hakikisha unafika kwenye ofisi ya Mtaa wako kuhakiki taarifa hizo.
ubungomanispaa
www.ubungomc.go.tz


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
SHUKRANI
Viongozi,Madiwani na Menejimenti ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo wanatoa shukrani zao za dhati kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha shilingi 176,358673.90/= kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi la Operesheni Anwani za Makazi na Postikodi.
NJETENI ROAD
LUGURUNI ROAD
ASANTE
Mhe. Rais Wetu
Samia Suluhu Hassani
KAZI IENDELEE.....!
Ubungo yetu fahari yetu
www.ubungomc.go.tz


'Safisha,Pendezesha, Ubungo'
"Ubungo kuwa na Muonekano wa Kijani"
02 Desemba,2021
Kila Mtaa uweke lengo la idadi ya miti inayotakiwa kupandwa kwa kila nyumba ili kuwa na Ubungo ya kijani
'Ubungo yetu fahari yetu'
www.ubungomc.go.tz


JENGO BORA
UTAWALA BORA
'Ubungo yetu fahari yetu'
www.ubungomc.go.tz


Miaka
60
YA UHURU WA
TANZANIA
1961-2021
Ubungo yetu fahari yetu
www.ubungomc.go.tz


14 OCT
2021
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
Miaka
—22—
Kumbukumbu ya
Mwl.Julius K. Nyerere
1922-1999
Ubungomanispaa


22 OCT
2021
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
"Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ya shinda tuzo ya Matumizi BORA ya TEHAMA kwa mwaka 2021"
"TEHAMA NI MSINGI WA TAIFA ENDELEVU"
"Ubungo ya kidigitari"
Ubungo yetu, fahari yetu.
Ubungomanispaa




OFISI ZA MANISPAA YA UBUNGO
ZILIZOPO LUGURUNI



KAMISAA WA SENSA - TAIFA AKIWASILI KATIKA OFISI YA MKUU WA WILAYA UBUNGO KWA AJILI YA KIKAO KAZI CHA SENSA YA MAJARIBIO



DARAJA LA JUU LA KIJAZI

KIJAZI INTERCHANGE




KITUO CHA MABASI CHA MAGUFULI



**KATIBU MWENEZI WA CCM TAIFA, ndugu, SHAKA HAMDU SHAKA AKIWA KATIKA ZIARA YA UKAGUZI WA MRADI WA KITUO CHA MABASI CHA MAGUFULI.**







**WAZIRI WA OFISI YA RAIS TAMISEMI MHE. INNOCENT BASHUNGWA AKIWA KATIKA ZIARA YA KIKAZI ALIYO IFANYA KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO KWENYE MRADI WA KITUO CHA MABASI CHA MAGUFULI.**





# KAMATI YA BUNGE YA MAZINGIRA YAFANYA ZIARA UBUNGO

















**WAJUMBE WA KAMATI YA MIPANGO MIJI MANISPAA YA UBUNGO, WAMETEMBELEA KITUO CHA UCHAKATAJI WA TAKA KILICHOPO BONYOKWA KINACHOJULIKANA KAMA MATERIAL RECOVERY FACILITY CENTER (MRF)**

## UZINDUZI WA CHANJO YA POLIO HOSPITALI YA SINZA PALESTINA

Ubungo imezinduzi rasmi zoezi la utoaji wa chanjo ya polio katika Hospitali ya Sinza Palestina ikiwa ni awamu ya tatu ya utoaji wa chanjo hiyo na zoezi Hilo litaendelea kufanyika kwa muda wa siku nne kuanzia tarehe 1 Hadi 4 septemba, 2022

Kwa Wilaya ya Ubungo watoto 174,588 wanalengwa kufikiwa na Katika kuhakikisha huduma inawafikia wananchi kwa haraka. Wataalamu wa Afya watapita nyumba kwa nyumba na pia katika Vituo vyote vya Afya chanjo tayari imesambazwa.

Uzinduzi wa zoezi hilo ulifanyika tarehe 1 septemba, 2022 ambapo Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mheshimiwa Kheri James aliwasihi Wakina mama kuhakikisha watoto wanapata chanjo hiyo kuwaepusha watoto na ugonjwa wa kupooza

"Wananchi wetu tutawafikia popote walipo, wahudumu wetu wa Afya watapita kuhakikisha zoezi hili linafanyika" alisema hayo Kheri

Kheri Aliendelea kuwasisitiza wakina mama hao kuhakikisha wanazingatia usafi wa maeneo yao kwa kunawa mikono na maji safi na kuweka makazi yao safi ili kuwalinda watoto dhidi ya ugonjwa wa Polio na maradhi mengine yanayosababishwa na uchafu.



## IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI MANISPAA YA UBUNGO





Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi Manispaa ya Ubungo Selemani Kateti amefanya kikao na watumishi walio chini ya Idara ya Utawala na Utumishi na kuwakumbusha utekelezaji wa majukumu yao wanapokuwa katika Ofisi zao kwa kusimamia majukumu yao na kufata kanuni, taratibu na Sheria za kazi

Kikao hicho kimefanyika Leo Agosti 10, 2022 ambapo Watumishi hao walipata nafasi ya kushiriki kutoa Mapendekezo na maoni mbalimbali ili kuimarisha utendaji kazi

Kateti, aliwataka watumishi hao Kila mmoja kujua nafasi yake anapokuwa katika kituo Chake Cha kazi ili kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma .

"Tujifunze kujiamini na mkasimamie ipasavyo watu mnao waongoza katika Vituo vyenu vya kazi" aliongeza Kateti.

Aliendelea kwa kusisitiza Kila mmoja kushiriki katika maswala ya kijamii ili kupeana nguvu na faraja mtu anapopata changamoto na hata matukio ya furaha.

Aidha, Kateti alisema pia ushirikiano ni muhimu, upendo, kufata maadili ya kazi, kanuni, Sheria na taratibu za kazi ni Jambo la msingi Kwakila mmoja wetu kuzingatia.

Katika swala la ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri watendaji waliomba ushirikishwaji wa maafisa biashara ili kufanya kazi kwa pamoja na kuomba uwepo wa kikao cha tathmini ambacho kitalenga kuboresha na kuongeza mapato ya Halmashauri.

Aidha, watumishi hao walimpongeza mkuu wa idara hiyo kwa kusimamia vyema changamoto wanazozipata na kuahidi kuendelea kufanya kazi kwa uweledi.



# MHESHIMIWA YUSUPH OMARI YENGA NAIBU MEYA MPYA UBUNGO.



YUSUPH OMARI YENGA diwani wa kata ya Mburahati amekuwa naibu meya mpya wa Halmashsuri ya manispaa ya ubungo baada ya kushinda kwa kura 19 sawa na asilimia 95% akichukua nafasi ya aliyekuwa Naibu Meya Mhe. Hassan Siraji Mwasha kutoka Kata ya Msigani baada ya kumaliza muda wake kwa mujibu wa sheria.

Uchaguzi huo umefanyika Leo agosti 15, 2022 ambapo Kila baada ya mwaka mmoja hufanyika uchaguzi kwaajili ya kumchagua Naibu Meya kwa mujibu wa Sheria.

Akitoa shukrani zake Mhe. YENGA ameshukuru wajumbe wa baraza hilo kwa kumpa kura za ndio

"Ntaenda kufanya kazi Kama mlivyoniamini, mnipe ushirikiano wenu" aliongeza Yenga

Nae aliyekuwa Naibu Meya Mhe. Hassan Mwasha ametoa shukrani zake za pekee katika baraza hilo kwa madiwani wote kwa ushirikiano mkubwa walio muonyesha kipindi alipokuwa Naibu na pia amempongeza Naibu Meya mpya kwa kupata nafasi hiyo.

Aidha, katika baraza hilo wenyeviti na wajumbe wa kamati mbalimbali walichaguliwa

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mheshimiwa Kheri James amempongeza kwa ushindi Naibu Meya YUSUPH OMARI YENGA na wajumbe wa kamati zote na kuwaahidi Serikali kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu

Nae Mkurugenzi wa Manispaa hiyo ndugu, Beatrice Dominic amewapongeza wajumbe wa kamati zote na Naibu Meya kwa kuchaguliwa na kuahidi kuendelea kushirikiana bega kwa bega katika kutekeleza majukumu ya halmashauri

Halikadhalika, Zoezi la ugawaji wa vyeti vya shukrani kwa waliokuwa viongozi wa kamati zilizopita lilifanyika.

Pamoja na hayo baraza liliwapongeza mtendaji kata ya Ubungo, Mwenyekiti sinza C, mtendaji kata ya manzese, Mwenyekiti Mtaa wa kibangu na Mwenyekiti wa Mtaa

# MAKALLA AMALIZA SINTOFAHAMU YA STENDI YA MAGUFULI NA STENDI BINAFSI

- Awataka LATRA kutokukwepa majukumu Na nyaraka zao walizotoa kwa stendi binafsi

- Aruhusu stendi binafsi 5 zilizohakikiwa Na LATRA kuendelea kutoa huduma Kwa sharti la kuingia na kutoka wapitie stendi ya Magufuli

- Aagiza Manispaa ya Ubungo kukaa Na wamiliki wa stendi binafsi kuona njia bora kukusanya mapato

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Amos Makalla ametangaza kuondoa katazo lililokuwa likizuia Mabasi yaendayo mikoani na nje ya Nchi kutoruhusiwa kupakia abiria au kushusha katika Vituo binafsi na badala yake ameruhusu utaratibu huo kuendelea Kwa sharti la kila basi kuingia ndani ya Kituo kikuu Cha Mabasi Cha Magufuli

RC Makalla ametoa maamuzi hayo wakati wa kikao Cha pamoja baina ya LATRA, Wamiliki wa Stendi binafsi na Halmashauri ya Ubungo na kubaini pasipokuwa na shaka kuwa Waliotengeneza Vituo binafsi walifuata taratibu na kupatiwa Vibali na LATRA Baada ya kukidhi vigezo

Miongoni mwa vigezo vilivyotolewa na LATRA ili kuruhusiwa kuanzisha Stendi binafsi ni pamoja na uwepo wa Vyoo, Sehemu ya mapumziko kwa abiria, viburudisho Na sehemu ya maegesho

Kutokana na Hilo RC Makalla ameridhia Vituo binafsi 5 vilivyohakikiwa kuendelea kutoa huduma na kufungua milango kwa wamiliki wengine wanaohitaji kuwa na Vituo binafsi kushirikiana na LATRA ili wapatiwe vigezo vinavyohitajika ambapo wamepewa Mamlaka ya kufuta au kutoa leseni

Aidha RC Makalla ameagiza Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kukaa kikao Mara moja na wamiliki wa Stendi binafsi ili kuona njia Bora ya ukusanyaji wa mapato










Ikiwa mwaka mpya wa fedha 2022/2023 umeanza tangu julai mosi, Halmashauri ya manispaa ya ubungo katika kufikia malengo ya kukusanya bilioni 32 kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani, watalaamu na viongozi kuanzia ngazi ya Mtaa wameamua kushirikiana bega kwa bega kukusanya mapato hayo na kufikia lengo.

Akiongea katika kikao hicho Mstahiki Meya wa Manispaa hiyo Mhe. Jaffary Juma Nyaigesha alieleza kuwa watendaji wa Kata na Mitaa wana jukumu kubwa la kuiwezesha Manispaa katika kufanikisha zoezi la ukusanyaji wa mapato kwani wanaostahili kuchangia mapato hayo ni wananchi na wafanya biashara ambao wapo katika mitaa yao.

Aidha Nyaigesha aliwasisitiza Viongozi hao kuhakikisha kuwa wafanya biashara na wananchi wote kwa ujumla wanalipa kodi, tozo, ushuru na ada mbalimbali za Halmashauri ili kuweza kuisaidia Manispaa hiyo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya Elimu, afya na masoko.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo Dkt. Peter Nsanya alisema kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 Manispaa ya Ubungo imekasimia kukusanya na kutumia kiasi cha shilingi Bilioni 32 kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani ikiwemo Ada ya Leseni, Ushuru wa Huduma na Vibali vya Ujenzi.

Nsanya amewataka watendaji hao kujua na kuainisha vyanzo wanavyopaswa kukusanya mapato kwenye maeneo yao na kuvisimamia ipaswavyo ikiwa ni pamoja na kuweka "target" za mapato wanayopaswa kukusanya ndani ya mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Nae Afisa Biashara wa Manispaa hiyo Bi Mary Mwakyosi ameainisha vyanzo vya mapato vya Manispaa hiyo kuwa Leseni za Biashara na za Vileo, Ushuru wa huduma, Vibali vya ujenzi na vya sherehe, Ada za taka ngumu na za ulinzi shirikishi, faini za kuvunja sheria na vinginevyo.

Kikao hicho kumeweka mikakati mbalimbali ikiwemo kuendelea kujenga uwezo kwa Watendaji wa Kata na Mitaa juu ya ukusanyaji wa mapato, kuwepo kwa Afisa biashara kwenye kila Kata, kutoa motisha kwa Mtendaji atakaefanya vizuri kwenye ukusanyaji wa mapato.

Manispaa ya Ubungo hiyo katika mwaka wa fedha uliopita wa 2021/2022 Manispaa hiyo ilikasiniwa kukusanya shilingi Bilioni 23 lakini ilifanikiwa kukusanya shilingi Bilioni 27 Sawa na asilimia 118%.

**WANANCHI NA WAFANYABIASHARA WOTE WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO MNAKUMBUSHWA KUENDELEA KUCHANGIA MAPATO YA MANISPAA KUPITIA VYANZO MBALIMBALI**

- USHURU WA HUDUMA
- LESENI ZA BIASHARA
- LESENI ZA VILEO
- VIBALI VYA UJENZI
- KODI MBALIMBALI
- VIBALI VYA MADINI YA UJENZI
- USHURU WA HOTELI
- ADA MBALIMBALI
- USHURU WA KUSHUSHA NA KUPAKIA
- VIBALI VYA SHEREHE

**ILI KUPATA TAARIFA MBALIMBALI ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO, WANANCHI NA WAKAZI WA MANISPAA YA UBUNGO MNAKUMBUSHWA KUFATA NA KUFATILIA KURASA ZETU ZA MITANDAO YA KIJAMII ZINAZOPATIKANA KWA JINA MOJA TU LA @ubungomanispaa**

*Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti yetu, www.ubungomc.go.tz*